


# Mojawapo Ya Misemo Ya 'MIMI NDIMI' Aliyotumia Yesu: "MIMI NDIMI MWANZO NA MWISHO"

Hujambo! Habari za asubuhi?

Tunapoendelea kuchunguza misemo ya Yesu kujihusu yeye mwenyewe, natumai unafuatilia kwa makini kila msemo na unaendelea kumwelewa zaidi.

Sasa tuangalie msemo mwingine wa Yesu anapojidhibitisha kubwa 'MIMI NDIMI';
Anasema 'MIMI NDIO MWANZO NA MWISHO'.

Katika Kitabu cha Ufunuo, Bwana Mungu anajitangaza kuwa 'Alfa na Omega', yaani 'Mwanzo na Mwisho'. Katika mwanzo wa ufunuo kwa Mtume Yohana anasema,

> **UFUNUO 1:8** *"Mimi ni Alfa na Omega, asema Bwana Mungu, aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi."*

Na mwisho wa Ufunuo Mungu anasema,

> **UFUNUO 21:6-7** *"Imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Kwa wenye kiu nitawapa maji bila gharama kutoka katika chemchemi ya maji ya uzima. Wale walioshinda watarithi haya yote, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watoto wangu."*

Katika Ufunuo, Yesu aliyefufuka na kutukuzwa anajilinganisha na Baba Mungu kwa kudai jina sawa:

> **UFUNUO 1:17-18** *Nilipomwona [Kristo Yesu], nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Kisha akaweka mkono wake wa kuume juu yangu na kusema: "Usiogope. Mimi ndiye wa Kwanza na wa Mwisho. Mimi ndimi Aliye Hai; Nilikuwa nimekufa, na sasa tazama, mimi ni hai milele na milele! Na ninazo funguo za mauti na kuzimu."*

Na katika mistari ya kumalizia ya Ufunuo Yesu aliyefufuliwa na kutukuzwa pia anabainisha yeye mwenyewe kama Alfa na Omega kwa kusawazisha misemo ya 'Alfa na Omega' na 'Mwanzo na Mwisho':

> **UFUNUO 22:12-13** *"Tazama, naja upesi! Ujira wangu u pamoja nami, nami nitatoa kwa kila mtu kulingana na yale aliyoyafanya. Mimi ni Alfa na Omega, wa Kwanza na wa Mwisho, Mwanzo na Mwisho."*

Je, Baba na Mwana wanamaanisha nini kwa kujiita 'Alfa na Omega'?

Katika alfabeti ya Kiingereza herufi ya kwanza ni "A" na ya mwisho ni "Z". Kwa hivyo tunaposema kutoka A hadi Z tunamaanisha kutoka mwanzo (wa Kwanza) hadi mwisho (wa Mwisho) na kila kitu kilicho katikati yake. Na hivyo vilevile Alfa (herufi ya kwanza ya alfabeti ya Kigiriki) hadi Omega (herufi ya mwisho) zinamaanisha kitu kimoja kama A na Z katika Kigiriki.

Kwa hiyo hii ina maana gani ya kivitendo kwetu sisi tunaoishi katika karne ya 21?

Kwanza, inamaanisha kwamba Baba na Mwana walikuwako kabla ya uumbaji wa kila kitu. Kama 'Alfa' walikuwepo wote toka mwanzo wa mambo yote. Waliutengeneza na kuujenga ulimwengu. Na wanaendelea kusimamia na kudumisha kila kitu kilichopo. *(Ona **Mwanzo 1**, **Yohana 1**, na **Wakolosai 1**)*

Baba na Mwana kama 'Alfa' (Wa kwanza) walianzisha kila kitu na tangu wakati huo wameandamana katika uumbaji, nyakati, na ubinadamu, mambo haya yote yanaposonga polepole kutoka Mwanzo kuelekea Mwisho.

Pili, ina maana kwamba historia ya mwanadamu na nyakati vina Mwisho, na Baba na Mwana (waliokuwa kabla ya mwanzo) pia wako Mwishoni wakingojea kuwasili kwako. Na zaidi, bado Baba na Mwana watakuwa hadi baada ya nyakati na maisha ya binadamu, ili kukamilisha makusudi yao.
*(Angalia **Isaya 51:6**, **Waebrania 1:10-12**, **2 Petro 3:10-12**, **Ufunuo. 6:12-14; 20:11**).*

Tatu, Baba na Mwana wanaishi katika kila kitu kati ya Alfa na Omega. Wanakaa kila mahali na wanaishi kila dakika katika nyakati zote.

Wanalenga kila wakati kuunda Watu wa kipekee wanaoitwa kwa majina yao - Watu wanaotambua na kuakisi utukufu wa Mungu - Watu ambao Roho wa Mungu huja kukaa ndani yao - sasa na hata milele.

Mungu alikufikiria muda mrefu kabla yako kutungwa mimba na kuzaliwa. Alitazamia siku hiyo atakapokuleta wewe ili utembee duniani; kumjua Yeye kama anavyokujua wewe.

Kwa hivyo ulikuwa sehemu ya mpango na kusudi la Mungu tangu mwanzo wa nyakati. Wewe sio ajali. Wewe sio makosa ya uhai. Wewe sio mdogo.

Ulileltwa kuwa sehemu ya mpango wa Mungu wa nyakati. Uliumbwa na kusudi kwa muda kama huu. Uliumbwa kwa ajili ya Mungu, na Mwana wake alifanywa kwa ajili yako.

Yesu ndiye mwandishi wa hadithi yako. Alikuwepo hapo mwanzoni mwako. Anakungoja mwisho wa maisha yako. Katika Roho wake Mtakatifu yuko pamoja nawe kila dakika. Hatakuacha kamwe.

Je, huyu ndiye Yesu unayemjua na kumpenda? Yesu unayemwabudu na kumtii? Yesu unayemtumikia na kumwakilisha? Yesu unayemtambulisha wengine?

Hakikisha unamfuata Yesu wa Biblia.

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.
Ni wako-




Douglas Van Devender.
Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.